



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA



Simu Na. 028-2520061  
Nukushi Na. 028-2520061  
Barua pepe: [info@geitadc.go.tz](mailto:info@geitadc.go.tz)  
Tovuti: [www.geitadc.go.tz](http://www.geitadc.go.tz)

**Septemba 16, 2024**  
**Geita**

**TANGAZO LA MAJINA YA MIPAKA YA KATA, VIJJI NA VITONGOJI KATIKA**  
**ENEO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA**

Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Halmashauri ya Wilaya ya Geita Ndg. Karia Rajabu Magaro leo **Septemba 16, 2024** ametangaza majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji ili kuwafahamisha Wananchi majina ya maeneo na mipaka ambayo itahusika katika kujiandikisha na upigaji wa kura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika **Novemba 27, 2024**.

Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina Majimbo mawili ya Uchaguzi ambayo ni Jimbo la Busanda lenye jumla ya Kata **22** na Tarafa **02** huku Jimbo la Geita likiwa na Jumla ya Kata **15**, Tarafa **02**.

Katika Kikao hicho kilichowakutanisha Watendaji wa Kata, Wajumbe wa Vyama vya Siasa, Wasimamizi wa Uchaguzi ngazi ya Halmashauri, Waheshimiwa Madiwani na Mwenyekiti wa Halmashauri, imeelezwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina jumla ya Tarafa **04**, Kata **37**, Vijiji **145** na Vitongoji **593**.

Pamoja na hayo Msimamizi wa Uchaguzi Ndg Karia Rajabu Magaro amewataka Watendaji hao kwa niaba ya Wananchi kubandika Tangazo hilo katika maeneo ya Ofisi za Kata na Vijiji.

Hivyo, kwa Mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2019 ibara 4(1-3) (Matangazo ya Serikali Na. 571, 572, 573 na 574) ya mwaka 2024, Msimamizi wa Uchaguzi anautangazia umma wa Watanzania na Vyama vyote vya Siasa vyenye usajili wa kudumu kuwa tarehe **27 Novemba, 2024** itakuwa ni siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Kwa Tangazo hili, Wananchi wote wanaombwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha, kupiga kura, kugombea na kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kupata Viongozi bora wa Serikali za Mitaa kwa maendeleo ya nchi yetu.

Imetolewa na:

Karia R. Magaro  
Msimamizi wa Uchaguzi  
Halmashauri ya Wilaya ya Geita